

**TANGAZO LA SERIKALI Na .....La Tarehe .....**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)**

**(SURA YA 288)**

**SHERIA NDOGO**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 89**

**SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI, 2019**

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

Jina na mwanzo 1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Afya na  
wa kutumika kutumika 1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Afya na  
Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya  
Lindi za Mwaka, 2019 na zitaanza kutumika baada ya  
kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini  
ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa  
vinginevyo:-

“Afisa Mwidhiniwa” Afisa yeyote wa umma  
atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji  
wa Sheria Ndogo hizi.

“Chakula” maana yake ni kitu chochote kinacholiwa na  
kunywewa na binadamu isipokuwa madawa, hii ni  
pamoja na:-

- (a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo  
ya chakula;
- (b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula;
- (c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula  
(binzari n.k);

“Choo cha kuvuta” maana yake ni choo ambacho  
kimejengwa na kuunganishwa na maji na kuwa na tanki  
ya kusukuma maji kwa ajili ya kuondoa uchafu hadi  
mahali palipoandaliwa;

“Choo bora” maana yake ni choo chochote cha maji  
chenye kuta na sakafu, banda imara la kudumu,  
limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa  
chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo

salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu, lenye vipimo vya futi 4 x 3 na kimo cha futi 12 na zaidi, au

“Choo cha Umma” maana yake ni choo kilichojengwa na Halmashauri au wakala wake kwa matumizi ya umma;

“Eneo la wazi” maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Lindi;

“Hati ya usafi” maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Kanuni za Afya.

“Jengo la biashara” maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kufanya biashara iliyokusudiwa.

“Kaya” maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba.

“Kero au chukizo” maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha:-

- (a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu.
- (b) harufu mbaya na kuudhi.
- (c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile nzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;
- (d) magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, nzi, panya na viumbe wenye madhara;

“Kituo cha taka” maana yake ni kizimba cha taka (collection center) kilichowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye dampo la taka ngumu la Halmashauri.

“Maegesho” maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha vyombo vya

usafiri kwa muda ambayo taasisi zingine za serikali hazina mamlaka nazo katika utozaji utozaji wa ushuru wa maegesho.

“Maji taka” kama ilivyo katika Sheria ya Mazingira 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwandani.

“Mazao au mimea marefu” maana yake ni mazao au mimea inayozidi sentimita 15 kwenda juu kama vile Mtama, Mihogo, Mahindi, Mbaazi, Uwele na mengine yote yale yanayofanana na hayo;

“Mkazi” maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri.

“Mmiliki” maana yake ni mtu yeyote ambaye ana miliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote katika mtaa, endapo mazingira husika ni mtaa au barabara za mtaa;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“Mzalishaji wa taka ngumu” maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara, kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake huzalisha taka.

“Pipa la taka” maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira.

“Taka” kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka.

“Taka Ngumu” kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa mazingira, 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani, katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo,

pamoja na taka za vyakula, karatasi plastiki au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps).

“Taka za Majumbani” maana yake itajumuisha mabaki ya chakula, maganda ya matunda, majivu, kinyesi cha mifugo, taka za bustani, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa.

“Taka za Viwandani” kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 sehemu ya IX.

“Taka Hatarishi” kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira Na 20 ya mwaka 2004, maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, hospitalini au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira.

“Uchunguzi wa Afya” maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vimelea vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi.

“Ufugaji wa ndani” maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya eneo lililoruhusiwa tu.

“Ukanda wa Mjini” unajumuhisha kata ya Makonde, Rahaleo, Mikumbi, Mitandi, Mwenge, Wailes, Ngoro, Msinjahili, Nachingwea, Matopeni, Mtanda, Rasbura, Mnazimmoja na Mingoyo.

“Ukanda wa Kijani” unajumuhisha kata ya Mbanja, Jamhuri, Kitumbikwela, Chikonji, Ng’apa na Tandangongoro.

“Vyakula vya kupikwa au kukaangwa” maana yake ni nyama, wali, ndizi, ugali maandazi, vitumbua, hilling, mikate, samaki, chipsi, kuku na vinginevyo

“Wakala” maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha

watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA PILI

### USAFI WA MAZINGIRA

- Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira 4. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki eneo la nyumba kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake kwa kuhakikisha kwamba;
- (a) majani yanayozunguka nyumba yake yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake;
- (b) taka taka zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;
- kushiriki shughuli za usafi wa mazingira 5. (1) Kutakuwa na siku maalum ambayo Halmashauri itatenga kwa lengo la wananchi kufanya usafi kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi na biashara zote zitafungwa wakati wa zoezi la usafi.
- (2) Itakuwa ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha kwamba anashiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika siku maalum zilizopangwa na Halmashauri na mwananchi atakayekataa kushiriki katika shughuli za kufanya usafi atakuwa ametenda kosa.
- (3) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara.
- Mimea mirefu Manispaani 6. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo ya Manispaa pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa na Halmashauri.
- Usafi wa mifereji ya maji ya mvua. 7. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya nyumba yake au

			eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mfereji huo unakuwa msafi, na imara siku zote.
Uwekaji taa za nje ya nyumba	8.		Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba, mpangaji au mfanyabiashara kuweka taa yenye mwanga nje ya jengo analoishi au analolitumia kwa shughuli yoyote na atatakiwa kuiwasha wakati wa usiku.
Kupaka rangi majengo	9.		Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kwamba anapaka rangi nyumba yake au duka lake ndani na nje kila itakapochakaa.
Wajibu kuondoa kudhibiti mazalia mbu.	10.	wa na ya	Itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa nyumba kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.
Biashara matunda	11.	ya	(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara ya matunda kuhakikisha kuwa ana chombo maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda. (2) Ni marufuku mtu yeyote kufanya biashara ya matunda pembeni mwa barabara au katika maeneo yasiyoruhusiwa.
Upulizaji dawa	12.		Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upuliziaji dawa "Fumigation" au biashara ya kuua wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na awe na leseni hai kutoka Halmashauri.
Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo	13.		(1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.
Kuegesha magari mabovu			(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha gari bovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi, barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo. (3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo.

### SEHEMU YA III

#### UIMARISHAJI WA AFYA

- Usalama wa maji kunywa. 14. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba anachemsha na kuchuja maji yote yanayotumika kwa kunywa ili kuyafanya yawe safi na salama bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.
- Utengenezaji, na uuzaji vyakula. 15. (1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza, kuchoma, kupima, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya na amepata kibali kutoka Halmashauri.
- Uuzaji vyakula vilivyopikwa. (2) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia nzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya kwa binadamu.
- Usalama wa vyakula. (3) (a) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini;  
(b) vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza;
- Uzuiaji wa shughuli mbalimbali wakati wa Magonjwa mlipuko. 16. (1) Afisa Mwidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi, au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.
- Machinjio na maduka nyama. 17. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama (Butcher) kuhakikisha kwamba duka lake;  
(a) Ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu,  
(b) lina maji safi, magogo na misumeno ya kukatia nyama;  
(c) lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama; sehemu za mizani;  
(d) kuna pipa la kuhifadhia taka taka;  
(e) muuzaji ana vazi jeupe pamoja na Apron nyeupe;  
(f) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita

- Kuchinja na kuuza nyama mahali pasiporuhusiwa. 18. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja, au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.
- Ufugaji mijini 19. (1) Ufugaji unaoruhusiwa ni ule ambao hausababishi kero kwa majirani, yaani ufugaji wa ndani (zero grazing) kwenye zizi na kwa kuzingatia idadi ya mifugo inayoruhusiwa au katika maeneo yaliyotengwa kama malisho ya mifugo.
- (2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuachwa kuzurura hovyoya mitaani, barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa.
- Usafi wa zizi 20. Itakuwa ni wajibu wa kila mfugaji kuhakikisha kwamba sehemu anayotumia kufugia;
- (a) inakuwa katika hali ya usafi wakati wote;
- (b) anakusanya uchafu wowote utokanao na wanyama kama vile kinyesi, manyoya na nyasi au mabaki ya vyakula na kwenda kutupwa kwenye dampo au kupelekwa shambani kama mbolea.
- Upimaji wa afya 21 (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mhadumu wa hoteli, mgahawa, baa, bucha sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza kupima afya zao kila baada ya miezi sita na watalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu tano (Tsh.5, 000/=).
- (2) Mmiliki yeyote atakayeruhusu mhadumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (Tsh. 50,000).
- Uwezo wa kukagua. 22 (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote wakati wa saa za kazi kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
- (2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

### **SEHEMU YA III**

### **UTUPAJI TAKA**



- Wajibu wa Halmashauri 23. (1) Halmashauri itatenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka (dampo) na kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji hadi kwenye dampo, Isipokuwa mmiliki wa kiwanda atakuwa na wajibu wa kuzoa taka zitakazozalishwa katika kiwanda chake na kuzitupa katika eneo lililotengwa (dampo).
- (2) Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii (CBOs) na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.
- Wajibu wa kuwa na pipa la taka 24. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba, mpangaji, mfanyabiashara au taasisi kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhi taka ngumu kabla ya kupelekwa kwenye kizimba au kuchukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa.
- (2) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba anatupa uchafu, taka, maganda ya matunda, mabaki ya vocha za simu katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.
- (3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka au uchafu wowote au kuacha kuwepo takataka au uchafu kwenye nyumba, uchochoroni, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.
- Uhifadhi maji taka 25. (1) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.
- Kutiririsha maji taka 26. Ni marufuku kutiririsha au kuelekeza maji, kutoka vyooni, bafuni, karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, meneo ya wazi, mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.
- Taka za viwanda 27. (1) Itakuwa ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo la Halmashauri.
- (2) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka

nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe wengine hai.

Uendeshaji wa 28.  
viwanda

Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

Ada ya uzoaji 29.  
taka

- (1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji wa taka kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi.
- (2) Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.
- (3) Bila kuathiri kifungu kidogo cha kwanza katika kifungu hiki tozo ya uzoaji wa taka itajulikana kama tozo ya matumizi ya dampo kwa wamiliki wa viwanda au mzalishaji taka kutoka viwandani.
- (4) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Uteuzi wa 30.  
wakala

Halmashauri inaweza kuteua kampuni, kikundi, kikundi cha jamii au Mtu binafsi kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA IV

### UJENZI NA MATUMIZI YA VYOO

Wajibu wa 31.  
kuwa na choo  
na kukitumia

- (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.

Umbali wa  
kujenga choo

- (2) Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya Nyumbani.

- Vyoo vya umma 32. (1) Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya Umma (Public toilet) katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.
- (2) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika mkataba wake na mawalaka watakaopewa jukumu la kusimamia vyoo hivyo.
- Vyoo vya muda katika mikusanyiko 33. Itakuwa ni wajibu wa mtu, kikundi, Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya ujenzi, sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri
- Vyoo katika majengo ya biashara 34. Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo viwili vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya matumizi ya jinsia za kike na kiume.
- Ilani ya kujenga choo 35. (1) Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo, choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.
- (2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa.
- Ilani ya kuondoa kero 36. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji, na, au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.
- (2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.
- Mkurugenzi kuteua mkaguzi 37. Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kuwa mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usafi katika eneo la Halmashauri.
- Makosa 38. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;

- (a) atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi; au
- (b) atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi,
- (c) atamwaga takataka katika mtaa, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote la wazi bila idhini ya Halmashauri;
- (d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;
- (e) atatirirsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;
- (f) ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;
- (g) atauza vyakula vilivyopikwa barabarani au nje ya majengo mengine;
- (h) atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, hifadhi ya barabara, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;
- (i) atanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba au maeneo ya makazi;
- (j) ataenda haja ndogo au kubwa hovyoo barabarani, uchochoroni, upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni.
- (k) atashindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

Adhabu	39.	Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shillingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yani faini na kifungo.
Kufuta GN.58 ya 22/01/2016	40.	Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi GN. 58 la tarehe 22/01/2016

## JEDWALI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 29)*

### ADA YA UZOAJI WA TAKA

NA	AINA YA MAKAZI/BIASHARA	UKANDA WA MJINI ADA KWA MWEZI	UKANDA WA KIJANI ADA KWA MWEZI
1.	Bar au Club ya usiku	15,000/=	5,000/=
2.	Bucha	10,000/=	5,000/=
3.	Nyumba za kuishi (kwa kaya)	3,000/=	1000/=
4.	Watengeneza juice au barafu au bisi	1,000/=	500/=
5.	Mgahawa midogo/mama lishe n.k	2,000/=	1,000/=
6.	Migahawa (Café, Restaurant n.k)	25,000/=	5,000/=
6.	Wachoma , chips, nyama, kuku	5,000/=	1,000/=
7.	Zahanati za watu Binafsi	30,000/=	10,000/=
8.	Vituo vya afya vya watu binafsi	50,000/=	25,000/=
9.	Hospitali za watu binafsi	100,000/=	50,000/=
10	Groceries	10,000/=	5,000/=
11.	Maduka ya madawa	5,000/=	3,000/=
13	Vizimba au Vioski au meza za biashara	1,000/=	500/=
14.	Mafundi seremara au fanicha na magereji	30,000/=	15,000/=
15.	Wachomelea vyuma na vyuma chakavu	10,000/=	5,000/=
16.	Karakana na waosha magari, pikipiki na bajaji.	10,000/=	5,000/=
17.	Vyuo /shule za binafsi za bwani	20,000/=	20,000/=
18.	Vyuo /shule za binafsi za kutwa	10,000/=	10,000/=
19.	Maduka ya jumla	10,000/=	5,000/=
20.	Maduka ya rejareja	5000/=	3,000/=

21.	Magari yanayoshusha mizigo kwenye masoko kwa tripu	3,000/=	1,000/=
22.	Magari yanayoshusha mizigo sehemu za nje ya soko kwa tripu	2,000/=	1,000/=
23.	Boti inayoshusha mizigo/abiria mwaloni kwa safari	1,000/=	1,000/=
24.	Meli/vivuko za watu binafsi na Serikali	10,000/=	15,000/=
25.	Vilabu vya wauza pombe za kienyeji	3,000/=	2,000/=
26.	Saloon	5,000/=	2,000/=
27.	Nyumba za kulala wageni	6,000/=	3,000/=
28.	Wauza mkaa wa jumla	5,000/=	4,000/=
29.	Maduka ya vitabu na viandikia internet café	3,000/=	2,000/=
30.	Maduka ya vifaa vya ujenzi	5,000/=	3,000/=
31.	Vituo vya mafuta	15,000/=	15,000/=
32.	Mashine ya kusaga nafaka	5,000/=	3000/=
33.	Mashine ya kukoboa nafaka	5,000/=	3,000/=
34.	Wauza mbao	5,000/=	4,000/=
35.	Karakana za kuranda mbao	30,000/=	10,000/=
36.	Ofisi za binafsi	5,000/=	2,000/=
37.	Mafundi baiskeli	1,000/=	500/=
38.	Wauza Mitumba	1,000/=	500/=
39.	Wauza mitumba nje ya soko	1,000/=	500/=
40.	Wauza nafaka	3,000/=	1,000/=
41.	Waziba pancha mitaani	3,000/=	500/=
42.	Wafuga kuku, ng'ombe, mbuzi etc kwa ajili ya biashara	4,000/=	2,000/=
43.	Viwanja vya ndege	100,000/=	100,000/=
44.	Viwanda vya samaki	25,000/=	15,000/=

45.	Bandari	15,000/=	15,000/=
46.	Viwanda vya kubangua korosho (kwa mahitaji)	100,000/=	100,000/=
47.	Viwanda vya kutengeneza maji ya kunywa	30,000/=	30,000/=
48.	Hoteli	30,000/=	30,000/=
49.	Taasisi za kifedha	15,000/=	15,000/=
50.	Makampuni ya Airtel, Vodacom, Tigo, Halotel	30,000/=	30,000/=
51.	Taasisi zingine au biashara zingine ambazo hazijatajwa hapa	20,000/=	20,000/=
52.	Pumba za mbao kwa trip -4.5m <sup>3</sup> -6m <sup>3</sup> -10m <sup>3</sup>	6,000.00/= 10,000.00/= 15,000.00/=	6,000.00/= 10,000.00/= 15,000.00/=
53.	Viwanda vidogo kwa trip -4.5m <sup>3</sup> -6m <sup>3</sup> -10m <sup>3</sup>	8,000.00/= 12,000.00/= 15,000.00/=	8,000.00/= 12,000.00/= 15,000.00/=
54.	Maegesho ya malori <b>i. chini ya masaa 6</b> -Lori chini ya tani 7 -Lori kuanzia tani 7 na zaidi <b>ii. zaidi ya masaa 6</b> -Lori chini ya tani 7 -Lori kuanzia tani 7 na zaidi	2,000.00/= 3,000.00/= 3,000.00/= 5,000.00/=	2,000.00/= 3,000.00/= 3,000.00/= 5,000.00/=
55.	Ada ya kutupa taka katika dampo kuu kwa siku -Lori chini ya tani 7 -Lori tani 7 na zaidi	20,000.00/= 30,000.00/=	20,000.00/= 30,000.00/=
56.	Usafirishaji wa taka rejeshi (Recycling) kwa safari	20,000.00/=	20,000.00/=

Nembo na mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 28 mwezi Januari, 2019.

.....  
*Jomaary M. Satura,*  
*Mkurugenzi,*  
***Halmashauri ya Manispaa Lindi***

.....  
*Mohamed L. Lihumbo*  
*Mstahiki Meya,*  
***Halmashauri ya Manispaa Lindi***

**NAKUBALI:**

.....  
*Suleimani S. Jafo (MB),*  
**WAZIRI OR - TAMISEMI**

**DODOMA**

Tarehe ...../.....2019